TANGAZO LA SERIKALI NA. 770 la tarehe 30/12/2022

SHERIA YA MISITU,
(SURA YA 323)

# NOTISI

(*Imetengenezwa chini ya kifungu cha 23(1)*)

## NOTISI YA KUSUDIO LA KUTANGAZA MSITU WA HIFADHI WA UVINZA KUWA MSITU WA HIFADHI YA MAZINGIRA ASILIA WA UVINZA YA MWAKA 2022

## UTANGULIZI

KWA KUWA Eneo la Msitu wa Hifadhi la Uvinza lilitangazwa chini ya kifungu cha 25 cha Sheria ya Misitu, Na. 30 ya mwaka 1957 kuwa Eneo la Msitu wa Hifadhi la Uvinza na kwamba lilichukuliwa kwa kuzingatia kifungu cha 108 cha Sheria ya Misitu, Sura ya 323 kuwa lilitangazwa hivyo chini ya Sheria tajwa;

KWA KUWA Waziri kwa mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 29 cha Sheria ya Misitu, Sura ya 323 anaona kwamba ni kwa maslahi ya umma kulipandisha hadhi Eneo la Msitu wa Hifadhi la Uvinza; na

NA KWA KUWA Waziri anatambua matakwa ya kifungu cha 29(2) cha Sheria ya Misitu ambayo, pamoja na masuala mengine, inamtaka Waziri kutoa notisi ya kusudio kwa umma kabla ya kutekeleza mamlaka hayo.

HIVYO BASI, Waziri anatamka kama ifuatavyo:

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kusudio la Kutangaza Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia wa Uvinza ya Mwaka 2022.

Eneo linalopendekezwa kutangazwa

2. Eneo la hifadhi ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali la Notisi hii linapendekezwa kutangazwa kama Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia wa Uvinza.

Madhumuni ya tangazo

3. Madhumuni ya kupendekezwa kutangaza Msitu wa Hifadhi wa Mazingira Asilia wa Uvinza kama Msitu wa Hifadhi wa Uvinza ni-

(a) kulinda eneo lililohatarini la misitu ya nyanda za chini za tropiki ambalo linatambulika kwa thamani yake ya juu ya baioanuwai, lenye upekee wa mimea na wanyama, ikijumuisha spishi za mimea na wanyama waliohatarini, baadhi yao wako katika hatari ya kutoweka; na

(b) kufikia malengo ya usimamizi yaliyokusudiwa, kulinda eneo la msitu na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu katika eneo la msitu.

Uhalali wa Notisi

4. Notisi hii itakuwa halali kwa muda wa siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa na ndani ya kipindi hicho mtu au kundi la watu au mwakilishi wao anaweza kwa maandishi-

(a) kupinga;

(b) kuwasilisha maoni; au

(c) kudai haki zozote zinazotokana na sheria za kimila,

kuhusiana na ardhi au mazao ya msitu au haki zozote zilizoainishwa kwenye sheria nyingine katika eneo ambalo linapendekezwa kutangazwa Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia wa Uvinza.

Uwasilishaji wa mapingamizi

5. Mapingamizi, maoni au madai yoyote dhidi ya tangazo la Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia wa Uvinza yawasilishwe ndani ya siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa Notisi hii kwa anauani ifuatayo:

Katibu Mkuu,
Wizara ya Maliasili na Utalii,
S.L.P. 1351,
DODOMA.

JEDWALI

*(Imetengenezwa chini ya aya 2)*


WILAYA YA UVINZA

MSITU WA HIFADHI YA MAZINGIRA ASILIA WA UVINZA

*Makadirio ya eneo:* Ekari 41,600 au Maili za Mraba 65

Unakopatikana na Mipaka

Eneo lote la hifadhi awali chini ya Eneo la Msitu wa Hifadhi wa Uvinza unaopatikana Wilaya ya Uvinza katika Mkoa wa Kigoma kama lilivyochorwa upya katika Ramani ya Idara ya Upimaji Na. Jb 3140 (Skeli 1:50,000) iliyohifadhiwa na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dodoma na lenye mipaka ifuatavyo:




Dodoma,
15 Desemba, 2022

PINDI H. CHANA,
*Waziri wa Maliasili na Utalii*